



Jina langu ni Koboole.
Ninaishi katika kijiji
kiitwacho
Mbalisana.



Siku moja nilikuwa
nikichuma matunda.
Nilishuhudia jambo
la kushangaza.



Niliona mistari
yarangi tofauti
angani.



Niliyaangusha
matunda niliyokuwa
nimechuma. Kisha,
nikakimbia
kuwaambia watu
nyumbani.



Niliwapata wakiwa wamesimama nje wakitazama juu kwa mshangao.



Nilisema kwa furaha, “Hii ni shuka maridadi.” Neno alinipinga akisema, “La! Hii ni rangi tofauti zinamwagika kutoka angani.”



Baadhi ya wanakijiji walikubaliana nami na wengine waliamini aliyosema Neno. Tulianza kubishana.



Wakati huo, mgeni mmoja alitokea na kusema, "Mmekosea nyote."



Tulipiga mayowe,
“Ikiwa tumekosea,
wewe tueleze
ukweli.”



Yule mgeni alisema,
“Mnachoshuhudia
ni upinde. Kwani
ninyi hamjawahi
kuuona upinde?”



Kwa mshangao
zaidi, tulimjibu, “La!
U-p-i-n-d-e ni nini?”



Neno alimwuliza,
“Je, huu upinde ni
wetu? Tunaweza
kuuweka hapa?”
Hatukupata majibu
kwa maswali yetu.
Mgeni huyo alikuwa
tayari ameenda
zake.